

FAHAMU HAKI ZAKO | Unaposimamishwa, Kukamatwa au Kuzuiliwa na Chombo cha Dola

<p>HAKI ZA JUMLA Unaposhughulika na Polisi au ICE</p>	<p>Ukaguzi: Hulazimiki kutoa ruhusa yaa kukagua mwili wako, mali zako au gari lako (isipokuwa kwa ukaguzi wa kimwili ikiwa kunashukiwa uwepo wa silaha).</p> <p>Ukikamatwa na Polisi: Ikiwa utakamatwa na polisi kwa uhalifu, una haki ya kupatiwa mwanasheria aliyeteuliwa na serikali ikiwa huna uwezo wa kuajiri mwanasheria.</p> <p>Ukizuliwa na ICE: Ikiwa umezuiliwa na ICE, una haki ya kupata ushauri kutoka kwa mwanasheria, lakini serikali hailazimiki kukupatia mwanasheria. Unaweza kuomba orodha ya wanasheria wanaotoa huduma bure/kwa gharama nafuu.</p> <p>Maswali ya Uhamiaji: Hulazimiki kujibu maswali kuhusu mahali ulipozaliwa, uraia wako, au jinsi ulivyoingia nchini (kanuni tofauti zinatumiwa kwenye mipaka, ikiwa ni pamoja na viwanja vya ndege). <i>Ikiwa wewe siyo raia na una umri wa miaka 18 au zaidi mwenye kadi ya kijani, viza halali au uthibitisho mwingine unaoonyesha uwepo wako halali nchini Marekani, lazima ubebe uthibitisho huo na huenda ukahitajika kuuonyesha ikiwa utaombwa na ofisa wa uhamiaji.</i></p>
<p>HAKI ZA DEREVA Wakati Unaposimamishwa Barabarani</p>	<p>Haki ya Kukaa Kimya: Una haki ya kukaa kimya. Ukichagua kutumia haki hii, itamke wazi kwa maafisa wa utekelezaji wa sheria.</p> <p>Hitaji la Kutoa Kitambulisho: Afisa anaweza kukutaka uonyeshe leseni yako, usajili wa gari au ushahidi wa bima na utaje jina na anwani yako au jina la mmiliki wa gari na anwani yake. <i>Kuendesha gari bila leseni kunaweza kuongeza nafasi ya kuzuiliwa.</i></p> <p>Maswali ya Uhamiaji: Hulazimiki kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji. <i>Tazama haki za jumla hapo juu.</i></p>
<p>HAKI ZA ABIRIA Wakati wa Kusimamishwa Barabarani</p>	<p>Haki ya Kukaa Kimya: Una haki ya kukaa kimya. Ukichagua kutumia haki hii, itamke wazi kwa maafisa wa utekelezaji wa sheria.</p> <p>Hitaji la Kutoa Kitambulisho: Kwa kawaida hulazimiki kuonyesha kitambulisho chako ikiwa utaombwa na afisa. <i>Kukataa kuonyesha kitambulisho chako kwa kawaida siyo sababu ya kuzuiliwa, isipokuwa kama ofisa atatoa madai ya uwepo wa tuhuma za msingi kwamba unahusika katika uhalifu.</i></p> <p>Maswali ya Uhamiaji: Hulazimiki kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji. <i>Tazama haki za jumla hapo juu.</i></p>
<p>HAKI Ukiwa Umekamatwa au Umezuiliwa</p>	<p>Baki Kimya na Omba Upatiwe Mwanasheria: Sema kuwa unapenda kukaa kimya na omba upatiwe mwanasheria mara moja. Usifanue, kuweka sahihi au kuamua chochote kabla ya kupata ushauri kutoka kwa mwanasheria.</p> <p>Kupiga Simu:</p> <ul style="list-style-type: none"> Ikiwa utakamatwa na polisi, una haki ya kupiga simu ya ndani. Simu zinazopigwa kwa mwanasheria haziwezi kufuatiliwa na chombo cha dola. Simu zinazopigwa kwa mwanasheria haziwezi kufuatiliwa na chombo cha dola. <p>Taarifa za Uhamiaji: Kariri namba yako ya uhamiaji (Namba ya "A") na ishiriki na familia yako. <i>Hifadhi nakala ya nyaraka zako za uhamiaji kwa mtu unayeweza kumwamini.</i></p> <p>Wasiokuwa Raia na Wenye Hatia: Muulize mwanasheria wako jinsi hukumu ya jinai au maelezo ya mshitakiwa mahakamani yanavyoathiri hali yako ya uhamiaji. Usijadili hali yako na mtu yeyote isipokuwa mwanasheria.</p> <p>Ukiwa Gerezani/Umezuiliwa: Ofisa wa uhamiaji anaweza kukutembelea. Usijibu maswali au kuweka sahihi kwenye hati kabla ya kushauriana na mwanasheria. <i>Soma hati zote kwa umakini; omba upatiwe mkalimani unahitaji.</i></p>
<p>IKIWA HAKI ZAKO Zimevunjwa...</p>	<p>Andika namba za beji za maofisa, namba za magari ya doria, taasisi za vyombo vya dola na maelezo mengine. Pata taarifa za mawasiliano ya mashahidi.</p> <p>Tafuta matibabu mara moja kwa jeraha lolote na piga picha.</p> <p>Unaweza kuomba kuzungumza na mwanasheria. Ili kuelewa machaguo yako ya kisheria, unaweza:</p> <ul style="list-style-type: none"> Omba usaidizi kutoka ACLU ya North Carolina kwa kutumia fomu hii ya kuwasilisha maombi: acluofnc.org/intake Wasiliana na chama cha wanasheria cha jimbo ili upatiwe pendekezo la mwanasheria.

Ni muhimu kuelewa haki zako unapoingiliana na watekelezaji sheria (iwe polisi, ICE, au mamlaka zingine) bila kujali hali yako ya uhamiaji. **Kanusho:** Hii haijumuishi ushauri wa kisheria.